
# BWANA NI KARIBU NA WOTE

***Zaburi 144***

***Musique: Innocent BISHIKWABO***




1. Kila siku nataka kukusifu ee Bwana,
   Na kutukuza jina lako daima na milele.
   Bwana ni mkubwa wa kusifiwa sana,
   Wala ukubwa wake hauvumbulikani.

2. Bwana ndiye mwenye huruma na mpole,
   Mvumilivu na mwingi wa wema.
   Bwana ni mwema kwa wote,
   Na huruma yake ju ya kazi zake zote.

3. Bwana ni mwenye haki katika njia zake zote,
   Na mwema katika kazi zake zote.
   Bwana ni karibu na wote wanaomwita,
   Wote wanaomwita kwa uaminifu.